# TANGAZO

## KLINIKI YA ARDHI

Mkurugenzi wa Mji Korogwe kwa kushirikiana na Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Tanga anawatangazia wananchi wote wa mji wa Korogwe kuwa, kutakuwa na kliniki ya ardhi kwa muda wa siku mbili kuanzia tarehe 11/08/2025 hadi tarehe 12/08/2025 katika viwanja vya Shule ya Msingi Manundu Mazoezi(karibu na stendi ya zamani) kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi 10:00 jioni. Huduma zitakazotolewa katika kliniki hiyo ni pamoja na;

- Kusikiliza, kupokea na kutatua kero na malalamiko mbalimbali yanayohusu masuala ya ardhi.
- Ukadiriaji wa kodi ya pango la ardhi (kodi ya ardhi) utakaoenda sambamba na wateja kupatiwa bili kwa ajili ya kulipa kodi ya ardhi.
- Kupokea maombi ya kuandaliwa hatimiliki kutoka kwa wananchi wanaomiliki viwanja katika Mji wa Korogwe.
- Utoaji wa elimu inayohusu masuala ya ardhi, ikiwemo sheria za ardhi, haki na wajibu wa wamiliki wa ardhi. Elimu kuhusu namna ya mmikiki kutumia simu yake kukadiria na kujua deni lake la kodi ya ardhi pia itatolewa.

Karibuni tuwahudumie.

TOWN DIRECTOR
KOROGWE TOWN COUNCIL
KOROGWE

.............................................................

Happy Luteganya
**KAIMU MKURUGENZI WA MJI KOROGWE**

Scanned with CamScanner